MAONI YA JUMLA YA KUBORESHA MAPITIO YA SERA YA UKIMWI YA MWAKA 2001, YALIYOFANYWA NA AZAKI (ASASI ZA KIRAIA) KATIKA HOTELI YA BLUE PEARL – DAR ES SALAAM TAREHE 5/2/2010

Utangulizi

Tanzania AIDS Forum (TAF), kwa kushirikiana na Human Development Trust (HDT), SIKIKA na Action Aid Tanzania, waliandaa warsha ya kupitia Sera ya Taifa ya kudhibiti ukimwi ya mwaka 2001, kwa lengo la kuboresha na kuona kipi kinafaa kiendelezwe na kipi hakifai kiachwe. Warsha hiyo ilifanyika tarehe 5 Februari, 2010 katika hoteli ya Blue Pearl – Dar es Salaam.

Katika kutafuta maoni na ushiriki wa AZAKI zinazojishughulisha na mapambano dhidi ya virusi vya UKIMWI na UKIMWI, jumla ya Asasi za Kiraia ishirini zilishiriki mchakato huo.

Baada ya majadiliano na uchambuzi wa kina wa sera na kuzingatia suala la wakati, ikiwa pamoja na kufuata muongozo uliotolewa na Tume ya Taifa ya kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) jumla ya mapendekezo kumi na manne yaliibuliwa ambayo wadau wameona yataisaidia Kamati inayofanya mapitio ili kuboresha sera ya Taifa ya UKIMWI.

Mapendekezo ya wadau:-

1. Jina la Sera:

Inapendekezwa jina la sera liwe ni ***Sera ya Taifa ya kudhibiti Virusi vinavyosababisha Ukimwi.***

2. Takwimu za UKIMWI:

Inapendekezwa ziwekwe takwimu za hivi karibuni; mfano ziwekwe takwimu za tafiti zilizofanywa na Tume ya Kudhibiti UKIMWI wa mwaka 2007/08, na sio kuacha zilezile takwimu zilizopitwa na wakati.

3. Usiri:

Inapendekezwa kuwa kipengele kinachozungumzia usiri kipitiwe na kuangaliwa upya kwani usiri unachangia kuongeza maambukizi ya VVU na UKIMWI katika jamii.

4. Gharama zinazoambatana na huduma za kupima VVU na tiba ya ya UKIMWI:

Inapendekezwa kuwa huduma zinazoambatana na upimaji wa VVU pamoja na tiba ya UKIMWI zitolewe bila ya gharama yoyote (bure). Suala la uchangiaji limesababisha urasimu na mianya ya rushwa hivyo sera itamke bayana kabisa huduma hizi zitapatikana bure. Dawa zitolewe bila ya kutoa gharama yoyote.

Hii inatokana na ukweli kuwa upimaji na ushauri nasaha kwa sasa ni bure katika vituo vyote vya afya. Hivyo haina mantiki yoyote kwa sera kuongeza kipengele kinachoongelea uwezekana wa kuchangia gharama hizo kwani kipengele hiki kinatoa mwanya wa kutoza fedha kwa vituo vya afya vyenye lengo la kujifaidisha kifedha.

Sera itoe tamko la kuhakikisha matibabu ya VVU na magonjwa nyemelezi yanatolewa bila gharama na ni endelevu.

Aidha sera imetamka azima ya kuanzisha mfuko wa Ukimwi (sura ya 1.4), inashauriwa lisiwe wazo la kubuni tena bali liwekewe mkakati wa utekelezaji.

5. Upimaji VVU wakati wa ujauzito:

Sera ya UKIMWI ya mwaka 2001 (sura ya 6.11) inazungumzia upimaji wa Ukimwi kwa hiari wakati wa ujauzito. Hali halisi kwa sasa inaonesha upimaji wa VVU sio hiari kwa kina mama wakati wa ujauzito na matokeo ya vipimo yanamhusisha mama tu.

Inapendekezwa kuwa sera isijichanganye, iwe bayana kuwa upimaji VVU wakati wa ujauzito sio hiari, bali lazima na uwahusishe wazazi wote wawili (baba na mama) na sio mama pekee. Aidha msisitizo uwe wakati wote na sio wakati wa ujauzito peke yake.

6. Umri wa watoto yatima na wanaoishi kwenye mazingira magumu:

Inapendekezwa kutokana na hali halisi ya kitanzania watoto wengi wanakuwa hawajaweza kujitegemea hata pale ambapo wanapokuwa wamefikia umri wa miaka kumi na minane. Hivyo basi, umri wa watoto yatima na wale wanaoishi kwenye mazingira magumu uongezwe kufikia angalao miaka 21 badala ya wa ule wa sasa wa miaka 18.

7. Neno fedheha lisitumike badala yake Unyanyapaa:

Katika sura ya kwanza neno fedheha limetumika. Neno hili lina utata na haieleweki maana halisi ya neno hili ni nini. Hivyo basi inapendekezwa badala ya kuendelea kutumia msamiati huu ambao unaonekana kuwa na utata utumike msamiati *"Unyanyapaa"* ambao unaeleweka na kufahamika maana yake kitaifa na kimataifa.

8. Neno waathirika lisitumike bali litumike neno waishio na VVU:

Neno waathirika ni neno tata halimuainishi anayeishi na VVU na mtu mwingine aliyepata maafa. Hivyo inapendekezwa kuwa neno waathirika lisitumike, badala yake litumike neno "wanaoishi na VVU" (WAVIU).

9. Neno kusogeza siku liboreshwe iwe ni kuboresha afya ya aishie na VVU.

Neno kuongeza au kusogeza siku linaonekana kuwa sio sahihi kwani anayeweza kusogeza au kuongeza siku za mwanadamu ni Mungu pekee. Inapendekezwa kuwa neno sahihi la kutumika hapa liwe ni kuboresha afya ya anayeishi na VVU.

10. Neno jinsia tofauti litoke iwe kwa njia ya kujamiiana

Katika sura ya 2.3 neno jinsia tofauti limetumika. Inapendekezwa hapa lisiendelee kutumika bali litumike neno *"kwa njia ya kujamiiana"* pasipo kutofautisha jinsia.

11. Neno Mashirika yasiyo ya kiserekali:

Inapendekezwa neno Mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) libadilishwe na badala yake litumike Asasi za kiraia (AZAKi).

12. Mfumo wa Rufaa:

Inapendekezwa mfumo wa rufaa uboreshwe.

13. Haki ya watoto kupima VVU:

Kwa kuwa elimu ya ukimwi kwa sasa inatolewa hata kwa watoto, haina mantiki kuendelea kutaka ridhaa ya mzazi au mlezi ili mtoto kupima VVU. Sera itamke bayana kuwa watoto wana haki ya kupima afya zao ali mradi tu kanuni za ushauri nasaha zimefuatwa na kuzingatiwa. Hivyo basi mzazi au mlezi hatakuwa na haki ya kumzuia mtoto kupima afya yake pale yeye mwenyewe atakapokuwa anahitaji au inaonekana kwke kuwa inafaa.

14. Haki za walemavu:

Sera itambue haki za walemavu za kupata habari, elimu na kupima VVU. Mfano sera iweke wazi mikakati ya kuwasaidia walemavu, hususani machapisho ya wenye ulemavu wa kuona.

Tunaomba Kuwasilisha kwa Mchakato zaidi.